KCPE REVEALED NATIONAL EXAMINATIONS

Pinpoint Publishers
*Always to the point*

# KCPE REVEALED

## MTIHANI WA KITAIFA — KISWAHILI LUGHA— 2023

201504

Saa 1 Dak. 40

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika hii ya maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**

**JINA LAKO**

**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku nyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengewa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi **A, B, C, D**. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari kwenye kisanduku chenye herufi uliochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

23. Tegua kitendawili kifuatacho.
Ukimcheka anakucheka, ukimwomba anakuomba______
A. kioo B. mwangwi C. kivuli D. kasuku.

**Katika karatasi ya majibu,** jibu sahihi ni **B** mwangwi.

23. [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 23, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri, kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa.**

Pinpoint Publishers
*Always to the point*

*Email: info@pinpointpublishers.co.ke*

**FUNGUA UKURASA**

**Kuanzia nambari ya 1 hadi 15, soma vifungu vifuatavyo kisha ujibu kwa jibu lifaalo zaidi.**

__**1**__ usiku wa __**2**__ tulipogutushwa na __**3**__ wa ajabu. Mimi na baba yangu __**4**__ kuelekea upande __**5**__ magharibi. Umati wa watu __**6**__ pale. Waja wale walikuwa wamejihami kwa singe, mishale, mikuki na __**7**__. Nilipotupa jicho, niliona jitu __**8**__ na woja wale. Lilikuwa __**9**__ kwa wizi wa mifugo. Yamkini __**10**__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. Ilikuwa | B. Ulikuwa | C. Ilikua | D. Ulikua |
| **2.** | A. manane | B. machwa | C. manne | D. machweo |
| **3.** | A. mayoe | B. maajabu | C. unyende | D. shangilio |
| **4.** | A. tulitoka matiti | B. tulichana mbuga | C. tulienda tenge | D. tulitoka shoti |
| **5.** | A. ya | B. wa | C. kwa | D. ule |
| **6.** | A. walikuwa | B. ulikua | C. ulikuwa | D. tulikuwa |
| **7.** | A. bomu | B. mzinga | C. zeze | D. manati |
| **8.** | A. amezingirwa | B. limezingirwa | C. wamezingirwa | D. alizingirwa |

**9.** A. limetiwa mbaroni B. ametiwa mbaroni
C. limetiwa kapuni D. ametiwa pingu

**10.** A. umoja ni nguvu B. pwagu hupata pwaguzi
C. za mwizi ni arubaini D. uovu haulipi

Mwalimu ni ___**11**__ cha jamii. Bila mwalimu hatutakuwa na viongozi, madaktari mafundi, manahodha na __**12**__ ambaye huendesha garimoshi. Serikali yetu __**13**__ kuajiri walimu __**14**__ masomo yaendeshwe __**15**__ nchini kwetu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. kiongozi | B. kioo | C. kitovu | D. mkombozi |
| **12.** | A. mwalisaji | B. sarahangi | C. mhazili | D. kandawala |
| **13.** | A. ina budi | B. ina rasmali | C. haina budi | D. inayo hela |
| **14.** | A. ila | B. hili | C. ili | D. ilhali |
| **15.** | A. pote | B. mote | C. popote | D. kote |

***Chagua kiunganishi kifaacho.***

**16.** ___________ kusoma kwa bidii hakuupasi mtihani huo.
A. Ingawaje B. Almradi
C. Licha ya D. Pasi na

**17.** Tambua sentensi iliyotumia **"kwa"** ya kusudi.
A. Nimekula kwa kijiko.
B. Alienda moja kwa moja.
C. Nitamwendea kwa ushauri.
D. Tulishinda mabao sita kwa sufuri.

**18.** Maneno yaliyopigiwa vistari ni ya aina gani?
Mwanafunzi **mtiifu** amefaulu **yule** mwingine anacheza **sana**.
A. Kiwakilishi, kiashiria, kielezi
B. Kivumishi, kiwakilishi, kielezi
C. Kivumishi, kielezi, kitenzi
D. Kiwakilishi, kiashiria, kielezi

**19.** Pesa za kuanzisha biashara ni
A. riba B. mtaji
C. masurufu D. karadha.

**20.** Mstari wa tatu katika kila ubeti wa shairi la tarbia ni
A. utao B. mleo
C. ukwapi D. mloto.

**21.** Tambua vazi linavaliwa na wanawake pekee.
A. Kocho B. Bwelasuti
C. Bombo D. Kanchiri

**22.** Salamu zipi ni tofauti?
A. Umeshindaje
B. Sabalheri
C. Masalheri
D. Alamsiki

**23.** Neno **"shaghalabaghala"** lina silabi ngapi?
A. Sita
B. Tano
C. Kumi na mbili
D. Kumi na tano

**24.** **Andika udogo wa:** Jiwe lilimgonga mwizi akaanguka.
A. Jijiwe liligonga jizi likaanguka.
B. Kijiwe kilikigonga kijizi kikaanguka
C. Kijijiwe kilikigonga kijizi kikaanguka
D. Kijijiwe kiligonga kijizi kikaanguka

**25.** **Tegua kitendawili:** Anatembea juu ya miba ila hachomwi.
A. Kinyonga B. Nzi
C. Simba D. Ulimi

**26.** **Chagua usemi taarifa wa**
"Jana niliwapa kazi gani?" Mwalimu alimwuliza kiranja.
A. Mwalimu alitaka kujua kazi aliyowapa kiranja.
B. Mwalimu alimwuliza kiranja kazi aliyowapa.
C. Mwalimu alitaka kujua kutoka kwa kiranja kazi aliyokuwa amewapa siku iliyotangulia.
D. Kiranja aliuliza kazi waliofanya siku iliyotangulia.

**27.** Alama ya uakifishaji inayotumika kuonyesha maneno ambayo si ya lazima katika usemi ni
A. parandesi
B. ritifaa
C. alama ya hisi
D. alama ya mstari.

**28.** Chagua orodha ambayo ni visawe pekee.
A. mgunda, konde, zaraha
B. wadhifa, madaraka, cheo
C. siha, afya, sihi, buheri
D. banati, barabara, ghulamu, mvuli

**29.** Chagua semi ambayo haijaambatanishwa vyema na maana.
A. Zaliwa na nyota - kuwa na bahati nzuri
B. Kata kamba - kutoroka
C. Vaa miwani - kulewa
D. Kula mumbi - kosa ulichotarajia

**30.** Riziki ameolewa na Juma. Dadake Juma ni Ami. Je, Amina na Riziki wataitanaje?
A. Mwamu
B. Shemeji
C. Wifi
D. Mwanyumba

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40.</u>***

Bwana Shaka aliamua kugura nyumbani kwao na kujitoma jijini akiwa mwingi wa matumaini. Yamkini alikuwa ameona marika zake walioguria jijini wakinuka fulusi. Ukweli ni kwamba hakufahamu kuwa bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi. Alivutiwa na maisha walioishi waliotoka mjini. Aliifunga kazi yake ya kinyozi pale kijijini baada ya kukata shauri kuhamia mjini. Nia ilikuwa moja, kufanikiwa kama wenzake.

Aliabiri basi moja lililokuwa kuukuu. Hilo ndilo angeweza kwa sababu ya uchechefu wa fedha. Safari yenyewe ilikuwa ndefu na ya kuchosha. Ingemchukua takribani saa tisa njiani kabla ya kuonja mazingira mapya. Mle basini mlisheheni kelele za kila aina. Wakembe waliolilia maziwa ya mama zao. Wengine walikuwa wamechoka baada ya mwendo mrefu. Joto nalo lilizidi kuwatiririsha kijasho. Abiria wengine walibeba kuku ambao walizidi kukokoneka chini ya viti. Abiria wengine walionekana kutuama na kupiga soga bila kutatizika na kelele hizo.

Bwana Shaka alizamia mandhari ya nje kupitia dirishani. Yalimpa faraja ya moyo. Aliyekuwa kando yake alikuwa akiogolea katika bahari ya gonezi. Alikoroma huku udenda ukimtambalia kwenye shavu moja. Wengi wao mle walizamia rununu zao. Watabasamu kama wehu, wacheke kama waliopagawa, wanune hayo yote ni ya ulimwengu wa utandawazi. Matokeo na matukio mitandaoni ni ya kustaajabisha.

Safari iliyong'oa nanga saa thenashara ilifika katika mji wa Gugumia. Abiria walipelekwa katika mkahawa mmoja ili wajinunulie kishuka na hata kujinyosha kidogo. Licha ya hayo walielekezwa kwenye vyoo hasa kwa wale waliokuwa na haja. Shaka alipeleka mkono mfukoni. Akatoa vipeni vilivyosalia baada ya kulipa nauli. Vipeni vile vingekidhi hitaji la kushtaki njaa katika mikahawa kama ile ya watalii? Hakuwa na budi kuridhika kwa karanga au hindi la kuchoma. Wenye hela waling'ofua minofu ya mbuzi kwa wali au sima.

Wengine hasa watoto wakaagiza chipsi kwa nyama ya kuku. Hatimaye sharubali baridi shadidi ikasindikiza mlo huo tumboni.

Basi liliwasili jijini wakati wa alasiri. Bwana Shaka alifurahi kupokelewa na mwenyeji wake. Walielekea kwenye mtaa duni wa mabanda. Vyumba vya mabati kwenye mitaro ya maji machafu **vilimwacha** Shaka **kinywa wazi**. Alimfuata mwenyeji wake unyounyo pasi kufunua kinywa chake hadi kwenye safu ya vyumba vilivyokuwa upande wa kusini katika mtaa huo. Alibaki kama aliyepatwa na kitata kinywani, alipojaribu kuuliza mwenyeji wake. Majumba mazuri ya ghorofa yaliyomkaribisha baada ya kushuka kutoka basini yalionekana kwa mbali. Mvuto wa jiji ukayeyuka kama umande jua linapochomoza.

Waliketi sako kwa bako na mwenyeji wake. Wakazungumza. Akamweleza kuwa kazi mjini zimeadimika kama wali wa daku. Kazi ambayo **ingepatikana wakati huo ni ya kusukuma rukwama ili kuwauzia** wakazi wa mtaa jirani maji. Hakuyaamini macho na masikio yake lakini lisilo budi hubidi.

**31.** Aya ya kwanza inadokeza kuwa Bwana Shaka

A. alitoroka kwao
B. Shaka hakupendezwa na kwao
C. alijua bahati yake ni kuhamia mjini
D. alitaka kujilinganisha na marika.

**32.** Kwa mujibu wa aya ya pili

A. Shaka alipanda basi kwa sababu hakuwa na pesa
B. basi lilikuwa nafuu kusafiria
C. safari ndefu huhitaji basi ili usichoke
D. basi ndilo gari lililokuwa kwenye kituo cha kwao.

**33.** Abiria waliokuwa na utulivu mle ndani ni

A. waliokuwa na simu tamba
B. watoto wadogo.
C. waliokuwa wakipiga gumzo
D. waliokuwa wasinzia.

**34.** Kulingana na aya ya tatu

A. abiria jirani alikuwa akiogelea baharini
B. abiria waliokuwa na simu walifurahishwa na majirani
C. Bwana Shaka alifurahishwa na mazingira ya nje
D. Bwana Shaka aliudhika na abiria wengine.

**35.** Safari ya kuelekea jijini ilianza wakati gani?

A. Saa moja asubuhi
B. Jioni
C. Saa kumi na mbili asubuhi
D. Hatujaambiwa

**36.** Safari ilipofika katikati haya yote yalitendeka isipokuwa

A. kupumzika
B. kushtaki njaa
C. kutalii
D. kwenda uani.

**37.** Abiria walifika mji wa Gugumia wakati wa

A. adhuhuri
B. alasiri
C. magharibi
D. saa saba.

**38.** **"Sharubati baridi ilisindikiza huo tumboni,"** Hii ni fani gani?

A. Takriri
B. Tashbihi
C. Chuku
D. Tashihisi

**39.** Kazi mpya ya Bwana Shaka ilikuwa ya

A. kumbebea mwenyeji wake maji
B. kuwa mzegazega
C. kuuza maji mtaa wao mabandani
D. kusukuma mkokoteni mtaani.

**40.** Methali gani inaelezea hali ya mambo alipowasili mtaa wa mabandani?

A. Ukiona vyaelea jua vimeundwa
B. Mgeni njoo mwenyeji apone
C. Bahati ya mwenzio usilalie mlango wazi
D. Usilolijua ni usiku wa kiza

***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali 41 - 50.***

Maliasili ni vitu ambavyo vinatokana na maumbile vinavyopatikana katika mazingira au ardhini. Mifano ya maliasili ni misitu maji, madini, milima na manguka ya maji. Aghalabu vitu hivi huchangia katika kunawiri kwa nchi nyingi kiuchumi.

Misitu ni muhimu sana katika maisha ya waja na viumbe hai. Hii ni kwa sababu huhifadhi vyanzo vya maji kuboresha hali ya hewa. Aidha misitu hii huzuia mmomonyoko wa udongo. Kuni zinazotumiwa kutayarisha mapishi hutokana na misitu. Mbao zinazotumiwa katika ujenzi wa nyumba na madaraja hutokana na misitu. Dawa nyingi hutokana na mimea ambayo hupatikana misituni. Misitu ni makao ya hayawani na malisho ya mifugo. Vilevile, misitu huboresha shughuli za kilimo na kuboresha mandhari ya nchi yetu. Aidha misitu ni chanzo muhimu cha mapato kwa wananchi wengi.

Ni kutokana na umuhimu huo wa misitu serikali yetu imeweka mikakati kabambe kupigana na uharibifu wa misitu nchini. Mikakati hiyo ni kama dhidi ya wachomaji makaa, wakulima wanaokata miti kiholela ili kutekeleza shughuli zao za kilimo na majangili wanaowinda wanyama kwa viungo vyao muhimu.

Madini ni mojawapo ya maliasili muhimu sana. Nchi kama vile Afrika Kusini imepiga hatua kimaendeleo na kiuchumi kwa sababu ardhi yao imebarikiwa. Dhahabu ni yenye thamani kubwa. Haya ni madini yaliyo na rangi ya manjano ambayo hutumiwa kutengezea mapambo. Mengine yenye rangi bati ni fedha. Haya hutumiwa kutengeneza sarafu. Ya tatu yana rangi nyekundu au nyeupe na hutumiwa kutengenezea nyaya za umeme. Haya huitwa shaba. Madini magumu yaliyo na thamani sana ni almasi. Hayo hutumiwa kukatia vioo na madini mengine kuna alumini ambayo ni mepesi, rangi ya kijivu na fedha yanayotengenezea kikaango. Chuma ni madini magumu yanayotumiwa kujengea na kuundia vitu. Vilevile kuna choka, risasi, aloi na mengineyo.

Maji ni kitu kiowevu kisicho na rangi maalum. Maji hutokana na mvua, bahari, maziwa, mito, chemichemi na visima. Maji ni maliasili muhimu sana katika maisha ya binadamu na hayawani. Binadamu hutumia maji kwa njia mbalimbali ambazo nina hakika unazifahamu.

Milima na mabonde ni muhimu sana. Katika vilele vya milima mingi kuna theruji. Theruji husababisha mzizimo au baridi shadidi kule juu. Milima hii huchangia ukuaji wa uchumi wetu. Watalii hutoka Ughaibuni kuja kuzuru sehemu hizi ambazo vivutio vikuu. Maanguko na maporomoko ya maji vilevile huwavutia watalii kutoka mataifa mbalimbali. Pesa wanazolipa hutumiwa na serikali kuboresha miundo msingi, elimu na hata kugharamia dawa hospitalini.

Ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha kuwa tunu hii tuliopewa na Mola imetunzwa na kutumiwa ifaavyo, la sivyo hatutaona umuhimu wake.

41. Kulingana na aya ya kwanza, mara nyingi

A. maliasili hutokana na maumbile
B. maliasili ni misitu, madini, maji, milima na maporomoko ya maji
C. uchumu uboreshwa kutokana na maliasili
D. kunawiri kwa nchi yoyote kunategemea maliasili tu

42. Ni gani huhifadhi vayo vya maji?

A. Misitu
B. Miti
C. Mito, maziwa na bahari
D. Milima

43. Kulingana na aya ya pili

A. Misitu huchangia mmomonyoko wa udongo
B. Misitu ndiyo maliasili muhimu zaidi
C. Dawa zote hutokana na miti misituni
D. Mazingira huonekana kuvutia palipo na misitu.

44. Misitu huboresha mazingira na
A. madhari
B. dawa
C. shughuli za zaraa
D. mifugo.

45. Ni ili haikutajwa kama chanzo cha uharibifu kulingana na aya ya tatu?
A. Kujenga nyumba
B. Kuchoma makaa
C. Wawindaji haramu
D. Ukulima

46. Nchi ambayo imepiga hatua kimaendeleo kutokana na madini ni
A. Kenya
B. Uganda
C. Afrika Kusini
D. Tanzania.

47. Madini ambayo hutumiwa kutengenezea pesa ni

A. dhahabu
B. shaba
C. almasi
D. fedha.

48. Taja madini ambayo mwandishi hakuelezea pekee
A. almasi, fedha
B. chumvi, bati
C. batikoa
D. shaba, chuma

49. Ni sekta gani haitegemei maliasili kulingana na kifungu?

A. Elimu
B. Kilimo
C. Usafiri
D. Viwanda

50. Ni methali gani inafaa aya ya mwisho?

A. Mjenga nchi ni mwananchi
B. Ukiona vyaelea jua vimeundwa
C. Ukuni mmoja hauwaki moto
D. Sheria ni msumeno hukata mbele na nyuma